TANGAZO LA SERIKALI Na………………..…. la tarehe………..………

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI,
(SURA YA 413)

KANUNI

(*Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 45*)

# KANUNI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA USIMAMIZI WA MADHARA YA UCHOVU KWA MADEREVA ZA MWAKA 2025

## MPANGILIO WA KANUNI


SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Kanuni Jina

1. Jina
2. Matumizi
3. Fasili

SEHEMU YA PILI
UELEWA KUHUSU MADHARA YA KUCHOKA

4. Zuio
5. Utimamu wa kufanya kazi
6. Masaa ya kazi na mapumziko
7. Muda wa juu zaidi wa Kuendesha
8. Hitaji la mapumziko ya lazima

SEHEMU YA TATU
MPANGO WA USIMAMIZI WA MADHARA YA UCHOVU

9. Mpango wa Usimamizi wa Madhara ya Uchovu

SEHEMU YA NNE
MAJUKUMU YA MTOA HUDUMA

10. Majukumu ya mtoa huduma
11. Takwa la dereva mwenza

SEHEMU YA TANO
MAJUKUMU YA DEREVA

12. Majukumu ya dereva

SEHEMU YA SITA
KUSIMAMISHA NA KUFUTA LESENI NA CHETI CHA UTHIBITISHO

13. Kusimamisha Leseni
14. Kusimamisha Cheti cha uthibitisho cha Dereva
15. Hatua za kusimamisha Leseni au Cheti cha Uthibitisho
16. Kufuta Leseni na Cheti cha Uthibitisho

SEHEMU YA SABA
MAKOSA NA ADABU

17. Makosa na Adhabu
18. Kufifilisha Makosa

SEHEMU YA TISA
MASHARTI YA JUMLA

19. Uelewa kuhusu madhara ya uchovu
20. Miongozo
21. Mapitio
22. Rufaa.

MAJEDWALI

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI
(CAP. 413)

KANUNI

(*Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 45*)

# KANUNI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA USIMAMIZI WA MADHARA YA UCHOVU KWA MADEREVA ZA MWAKA 2025

## SEHEMU YAKWANZA

## MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za mwaka 2025

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa-

(a) Dereva wa chombo cha huduma za usafiri wa barabara yanayodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini.

(b) Mtoa huduma anayetoa huduma za usafiri wa barabara zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhi.

Fasili

Sura ya 413

3. Katika kanuni hizi, isipokua muktadha utahitaji vinginevyo-

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Mamalaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini.

"safari ndefu" maana yake ni ni safari inayomuhitaji dereva kuendesha mfululizo zaidi ya saa nane

"mapumziko ya dereva" ni muda ambao dereva hutumia kwa mahitaji ya kibinafsi kama vile kwenda chooni na kula wakati wa safari;

"dereva mwenza" maana yake ni dereva anayechukua nafasi ya kuendesha chombo kutoka kwa dereva mwingine katika sehemu maalum ya kubadilisha kwa safari ndefu

"masaa za kuendesha" maana yake ni muda halisi wa dereva kuendesha,

"Kifaa vya Kielektroniki vya Utambulisho wa Madereva" maana yake ni kifaa chochote cha kielektroniki kilichoidhinishwa na Mamlaka kwa ajili ya kutambua dereva wa chombo cha usafiri kibiashara.

"uchovu" maana yake ni hali ya kuwa na usingizi, uchovu, au kuishiwa nguvu, na inajumuisha dalili za kutotulia, kuchoka, kutoweza kuendesha mwendo sahihi na macho yenye uchovu; na itajumuisha hali ya kuumwa, ushawishi wa dawa za kulevya au pombe na hali nyingine yoyote isiyofaa ambayo inaweza

kuharibu uwezo wa dereva kuendesha chombo kwa usalama."

**"**Mpango wa Usimamizi wa Madhara ya Uchovu" maana yake ni mpango wa usimamizi wa madhara ya uchovu unaoandaliwa andaliwa na mtoahuduma na kupitishwa na Mamlaka unaoonesha hatua za kuzuia madhara ya uchovu kwa madereva.

"Safari ndefu" maana yake ni safari ambayo dereva ataendesha gari kwa zaidi ya masaa nane mfululizo kwa siku;

"muda wa kutokuwa kazini" ni muda wa zaidi ya dakika 30 akiwa nyumbani, mbali na gari au akiwa safarini lakini katika sehemu ya kulala iliyofaa;
maana yake ni zaidi ya dakika 30 za mapumziko ya nyumbani, mbali na gari au, ikiwa ni safari ndani ya gari, kupumzika, kulala katika chumba cha kulala kinachofaa

"masaa ya mapumziko" maana yake ni muda ambao dereva anasimama kwa ajili ya kupumzika baada ya kuendesha gari mfululizo kwa muda ulioainishwa;

"chombo" maana yake ni chombo kinachoendeshwa kwa mitambo au umeme kilichokusudiwa kutoa huduma ya usafirishaji kibiashara

"masaa ya kazi" maana yake ni masaa ambayo dereva wa chombo cha kibiashara anatakiwa kufanya kazi kwa siku na yasizidi masaa 12; inajumuisha kuendesha gari na shughuli zote zinazohusishwa na kuendesha gari la biashara, muda uliotumika kupakia na kupakua, kukamilisha nyaraka, kujaza mafuta, kuangalia matairi, kufanya matengenezo, kusafisha gari, mapumziko ya chini ya dakika 30, kufanya mawasiliano na wasimamizi au madereva wengine kuhusu mipango ya kazi; na

"kitabu cha kazi" maana yake ni kitabu kinachorekodi madereva wakifanya kazi na saa za kupumzika.

## SEHEMU YA PILI

## KANUNI ZA USIMAMIZI WA MADHARA YA UCHOVU

Zuio

4.-(1) Dereva hataendesha chombo pale anapojua au kushuku kuwa anasumbuliwa na uchovu unaoweza kuhatarisha usalama wa chombo, abiria, watumiaji wengine wa barabara au miundombinu ya barabara.

(2) Mtoa huduma hatasababisha au kumruhusu dereva kuendesha gari pale anapojua au kushuku kuwa dereva anasumbuliwa na uchovu unaoweza kuhatarisha usalama wa vyombo, abiria, watumiaji wengine wa barabara au miundombinu ya barabara.

Utimamu wa kufanya kazi

5.-(1) Dereva atatakiwa kutoa taarifa juu ya utimamu wake baada ya kupumzika kwa muda unaohitajika na kuwa yuko sawa kuweza kuendelea na safari nyingine.

(2) Wakati wa dharura, dereva atatoa taarifa kwa mtoa huduma kwa kwa mujibu wa mpango wa dharura wa mtoa huduma ulioidhinishwa na Mamlaka.

(3) Mtoa huduma hatampanga au kumruhusu, na dereva hatakubali kazi ya kuendesha chombo pale ambapo ametoa taarifa ya uchovu.

(4) Dereva atathibitisha kwamba, hana hali ya uchovu wa kazi kabla ya

kuanza safari kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

Masaa ya kazi na mapumziko

6. Mtoa huduma na dereva wa chombo wanahitajika kuzingatia muda wa juu wa saa za kazi na ukomo wa chini wa saa za kupumzika kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 7 na 8 ya Kanuni hizi.

Muda wa juu zaidi wa Kuendesha

7.-(1) Dereva hataruhusiwa kuendesha chombo cha abiria kwa zaidi ya saa tisa ndani ya masaa ishirini na manne (24).

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), dereva hataruhusiwa kuendesha chombo kwa zaidi ya saa tano mfululizo bila kupumzika.

(3) Dereva hataruhusiwa kuendesha chombo kwa zaidi ya saa arobaini na nane (48) ndani ya siku saba mfululizo.

Hitaji la mapumziko ya lazima

8. Dereva atatakiwa kuchukua mapumziko ya lazima kama ifuatavyo:

(a) angalau saa kumi ndani ya masaa ishirini na manne (24);

(b) dakika thelathini (30) baada ya kuendesha kwa saa tano mfululizo; na

(c) masaa ishirini na nne mfululizo ndani ya siku saba za kazi.

## SEHEMU YA TATU
## MPANGO WA USIMAMIZI WA MADHARA YA UCHOVU

Mpango wa Usimamizi wa Madhara ya uchovu

9. (1) Mtoa huduma atatayarisha mpango wa usimamizi wa madhara ya uchovu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi na kuwasilisha kwa Mamlaka ili kuidhinishwa.

(2) Kwa kuzingatia yaliyoelezwa katika Kanuni (1), mpango wa usimamizi madhara ya uchovu utakuwa na angalau taarifa zifuatazo:

(a) jina la mtoa huduma;
(b) dhumuni na wigo wa mpango;
(c) utambuzi na tathmini ya hatari ya uchovu;
(d) mikakati ya kudhibiti uchovu;
(e) mipango ya mafunzo na uelimishaji;
(f) ufuatiliaji na utoaji taarifa kuhusu uchovu;
(g) ushughulikiaji wa matukio ya uchovu;
(h) utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka;
(i) mapitio na maboresho endelevu;
(j) Sehemu maalum za mabadiliko na mapumziko kwa madereva katika safari ndefu au muda mrefu wa kufanya kazi;
(k) muda na eneo maalum kwa ajili ya kubadilishana na mapumziko ya madereva ikiwa ni safari ndefu au muda mrefu wa kazi;
(l) hitaji la dereva kutumia vifaa vya kielektroniki vya utambuzi wakati wa kuanza, kubadilishana na kukamilika kwa safari.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), Mamlaka inaweza kuidhinisha, kupendekeza kuboreshwa au kukataa Mpango wa Usimamizi wa madhara ya uchovu

uliowasilishwa.

(4)Iwapo Mamlaka itatoa mapendekezo au kukataa mpango wa usimamizi madhara ya uchovu, itamjulisha mtoa huduma ndani ya siku saba za kazi na kueleza:

(a) mapendekezo ya kurekebisha; au

(b) sababu za kukataa.

(5) Ikiwa kutatokea mabadiliko yoyote kwenye mpango uliopitishwa, mtoa huduma atatakiwa kuwasilisha kwa Mamlaka na kupata idhini kabla ya kuanza utekelezaji wake

## SEHEMU YA NNE
## MAJUKUMU YA MTOA HUDUMA

Majukumu ya mtoa huduma

10. Mtoa huduma atakuwa na wajibu wa:

(a) Kuwa na dereva ambaye amethibitishwa, amesajiliwa na ana kitufe cha utambuzi kinachofanya kazi au alama ya vidole iliyotolewa na Mamlaka;
(b) kutoa kitabu cha kazi kwa dereva;
(c) kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Madhara ya Uchovu na kuuwasilisha kwa Mamlaka kwa ajili ya kuidhinishwa;
(d) kuandaa mpango wa kukabiliana na dharura
(e) kutekeleza Mpango wa Usimamizi wa Madhara ya Uchovu ulioidhinishwa na Mamlaka;
(f) kuhakikisha chombo kinawezesha matumizi ya kifaa cha ufuatiliaji mwenendo na kitufe cha Utambuzi wa dereva kilichoidhinishwa na Mamlaka
(g) kuhakikisha uwepo wa dereva mwenza katika safari ndefu kwa mabasi ya abiria na vituo vya kupumzika kwa madereva wa magari ya mizigo;
(h) kuhakikisha uwepo wa dereva mwenza kwa ajili ya kubadilishana iwapo vyombo vya kukodi, mabasi ya mjini na magari ya mizigo yanayofanya kazi kwa zaidi ya saa nane;
(i) kutompangia dereva wajibu wa kuendesha chombo ikiwa ametoa taarifa ya uchovu;
(j) kuhakikisha kuwa, Mpango wa Usimamizi wa Hatari ya Uchovu ulioidhinishwa umeambatishwa wakati wa kutuma maombi ya kufanya upya leseni;
(k) kuhakikisha kuwa dereva mwenza hayumo ndani ya gari lile lile linalotarajiwa kubadilishana iwapo magari yatakayopita katikati ya jiji.
(l) kuhakikisha kamera ya kugundua udhibiti wa uchovu imefungwa, inalindwa na inafanya kazi ipasavyo wakati wote;
(m) kusahisha na kutunza kumbukumbu zinazohitajika za kufuatilia saa za kuendesha gari na vipindi vya kupumzika; na
(n) kukagua utimamu wa madereva kabla ya kuanza safari.

Takwa la dereva mwenza

11.(1) Mtoa huduma atahakikisha kuwa dereva mwenza wa mabasi yaendayo masafa marefu atakuwepo kwenye kituo cha kubadilishana kwa ajili ya kupokea

basi,kutoka kwa dereva aliyeendesha kwa saa nane mfululizo kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Usimamizi Madhara ya Uchovu.

(2) Mtoa huduma atahakikisha kwamba dereva wa chombo vya kukodi, na magari ya mizigo na mabasi ya mijini anapata muda wa kupumzika au kubadilishana na dereva mwingine baada ya saa nane za kuendesha gari kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Kudhibiti Madhara ya Uchovu.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo (1) na (2), mtoa huduma atahakikisha kwamba wa chini wa saa za kupumzika kama zilivyoainishwa katika kanuni ya 8 ya Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TANO
## MAJUKUMU YA DEREVA

majukumu ya Dereva

12.- Dereve atakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) kutoa taarifa ya uchovu wakati hayupo timamu kuanza au kuendelea na safari nyingine.
(b) kudumisha na kuhakikisha matumizi sahihi ya Kitufe cha utambuzi cha dereva;
(c) kujaza taarifa sahihi kwenye kitabu cha kazi cha udereva;
(d) kuweka kumbukumbu ya kitabu cha kazi cha udereva;
(e) kukabidhi gari kwa dereva mwenza katika eneo lililoainishwa katika Mpango wa Kudhibiti Madhara ya Uchovu;
(f) kuzingatia kiwango cha chini cha saa za kupumzika kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi;
(g) kutoa taarifa muhimu kwa abiria walio ndani ya chombo kuhusu sehemu za kubadilishana/kupumzikia Madereva; na
(h) kujaza kwa usahihi fomu ya tamko la uchovu wa dereva.

## SEHEMU YA SITA
## KUSIMAMISHA NA KUFUTA LESENI NA CHETI CHA UTHIBITISHO

Kusimamisha Leseni

13. (1) Mamlaka inaweza kusimamisha leseni baada ya kujiridhisha kuwa a huduma amekiuka masharti yafuatayo kwa zaidi ya mara tatu kwa mwaka:

(a) kutozingatia utekelezaji wa Mpango wa usimamizi wa madhara ya uchovu ulioidhinishwa,
(b) kutokufunga na kufanya marekebisho ya kifaa cha kufuatilia mwenendo wa chombo ambacho kinaweza kutumia kitufe cha utambuzi wa dereva au alama ya kidole,

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), Mamlaka itasimamisha leseni pale ambapo mtoa huduma amekiuka masharti hayo kwa zaidi ya mara tatu kwa mwaka

Kusimamisha Cheti cha uthibitisho cha Dereva

14.- (1) Mamlaka inaweza kusimamisha cheti cha idhini cha udereva ikiwa imeridhika kwamba amekiuka masharti yafuatayo kwa zaidi ya mara tatu kwa mwaka:

(a) kutozingatia ukomo wa masaa ya kufanya kazi na muda wa kupumzika
(b) kutozingatia saa za ukomo wa juu wa kuendesha chombo mfululizo na

saa za ukomo wa chini wa kupumzika

(c) kutotumia kitufe cha kielektroniki cha utambuzi wa dereva au alama ya kidole

(2) Bila kuathiri kanuni ya (1) Mamlaka inaweza kusimamisha cheti cha uthibitisho wa dereva iwapo itaridhika kwamba amesababisha ajali na iliyopelekea uwepo wa vifo au majeraha makubwa kutokana na kukiuka Kanuni hizi.

Hatua za kusimamisha Leseni au Cheti cha Uthibitisho

15-(1) Mamlaka itasimamisha leseni ya chombo au cheti cha uthibitisho ya udereva baada ya kutoa notisi kuonyesha sababu kwa nini leseni yake ya chombo au cheti cha uthibitisho ya udereva kisisitishwe.

(2) Mwenye leseni au dereva anaweza, baada ya kupokea notisi chini ya kanuni ndogo ya (1) na ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kupokea notisi ya kuonyesha sababu, kufanya wasilisho la maelezo ya maandishi kwa Mamlaka.

(3) Endapo Mamlaka haijaridhika na maelezo yaliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (2) au mwenye leseni au dereva hajatoa wasilisho lolote, Mamlaka inaweza kusimamisha leseni au cheti cha uthibitisho na kutoa sababu za kufungiwa.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), (2) na (3), Mamlaka inaweza, kwa maslahi ya usalama wa umma au usalama kuhusiana na usafiri wa barabarani, kusimamisha leseni au cheti cha Uthibitisho cha dereva bila takwa la kupata maelezo ya kuonyesha sababu ya kufanya hivyo kutoka kwa mwenye leseni au dereva.

(5) Endapo leseni au cheti cha uthibitisho kimesitishwa chini ya Kanuni hizi, mwenye leseni au cheti cha Uthibitisho wa dereva ataacha mara moja kutoa huduma ya usafiri wa umma na ataikabidhi leseni au cheti cha Uthibitisho wa dereva kwa Mamlaka ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kupokea taarifa ya kusimamishwa.

(6) Mamlaka inaweza kurudisha leseni au au cheti cha Uthibitisho kwa mwenye leseni na cheti baada ya kumalizika kwa muda wa kusimamishwa na kufuata masharti yaliyoainishwa katika notisi ya kusimamishwa.

Kufuta Leseni na Cheti cha Uthibitisho

16. Mamlaka inaweza kufuta leseni iliyosimamishwa au cheti cha au cheti cha Uthibitisho wa dereva chini ya Kanuni hizi iwapo itaridhika kuwa mwenye leseni ni mkosaji wa mara kwa mara au anahatarisha usalama wa umma.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na Adhabu

17.(1) Mwenye leseni atakayekiuka mojawapo ya masharti ya Kanuni hizi, atakuwa ametenda kosa na akikutwa na hatia, atalipa faini isiyopungua shilingi laki mbili za Tanzania lakini isiyozidi shilingi laki tano; au kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

(2) Dereva atakayekiuka mojawapo ya masharti ya Kanuni hizi, atakuwa ametenda kosa na akikutwa na hatia, atalipa fainifaini isiyopungua shilingi laki moja lakini isiyozidi shilingi laki mbili za Tanzania; au kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha makosa

T.S Na. 19 la 2024

18.-(1) Mamlaka inaweza, pale mtu anapokiri kwa maandishi kwa Mamlaka au afisa wake aliyeidhinishwa kuwa ametenda kosa, afisa aliyeidhinishwa wa Mamlaka anaweza, wakati wowote kabla ya kuanza kusikilizwa kwa kesi na Mahakama yenye uwezo, itajumuisha kosa hilo kwa namna iliyoainishwa katika Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Ufifishaji wa Makosa).

(2) kiasi kinachojumuishwa kitalipwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI YA JUMLA

Uelewa kuhusu madhara ya uchovu

19. Mtoa huduma na dereva wanalazimika kuwa na maarifa ya kimsingi kuhusu sababu zinazoweza kupelekea uchovu na namna ya kuzuia kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne kwenye Kanuni hizi.

Miongozo

20.- (1) Mamlaka inaweza kutoa miongozo ya kuweka utekelezaji na ufuatiliaji wa Kanuni hizi amabyo itahusisha kutoa elimu kuhusu hathari za uchovu, usalama na utamaduni wa kuzingatia afya.

(2) Mamlaka inaweza kuandaa Miongozo ya namna ya kuwaongoza watoa huduma kwa kufuata Kanuni hizi

Mapitio
TS Na. 73 la 2020

21. Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na maamuzi ya Mamlaka chini ya kanuni hizi anaweza, ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya uamuzi huo, kuomba mapitio kwa Mamlaka kwa mujibu wa Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Kavu (Utaratibu wa Mapitio) za mwaka 2020.

Rufaa
Sura 285

22. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Ushindani, mtu yeyote ambaye hajaridhika na maamuzi ya Mamlaka anaweza kukata rufaa kwenye Baraza la Ushindani

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 5(4))*

FOMU YA MWONGOZO WA UDHIBITI WA HATARI ZA UCHOVU

- Dereva anatakiwa kuwa timamu ili kutekeleza majukumu yanayohitajika, kwa hiyo fomu hii ijazwe na kusainiwa na dereva mwanzoni mwa kila safari.
- Dereva atajaza fomu hii chini ya uangalizi au bila uangalizi wa msimamizi wake.
- Dereva anahitajika kujaza fomu hii kwa usahihi na kwa uaminifu.
- Dereva anayetoa taarifa za uongo ametenda kosa na akikutwa na hatia atawajibika kwa mujibu wa Kanuni hizi.

**a) Takwimu za dereva**

Jina la Dereva: ………………………………….
Na. ya leseni iliyoisha: ………………………….
Cheti cha Kuthibitishwa Na: …………...............
Tarehe ya safari ……..…………………..……………….…..
Muda ya kuanza safari: ……………….……….
Muda tarajiwa ya kumaliza safari: ……………..

**b) Taarifa za tamko**

Tafadhali weka alama ya (√) kwa kila kisanduku ili kuthibitisha taarifa zilizotolewa ni za kweli

☐ Nimelala na kupata usingizi kwa muda wa masaa sita au zaidi ndani ya masaa ishirini na nne yaliyopita
☐ Nimelala na kupata usingizi kwa muda wa masaa kumi na mbili au Zaidi ndani ya masaa arobaini na nane yaliyopita
☐ Nimepumzika kwa muda wa kutosha utakaoniwezesha kuendelea salama na safari siku ya leo
☐ Sijatumia pombe kwa muda wa masaa kumi na mbili yaliyopita
☐ Sina kiwango chochote cha pombe kwenye damu na sijaathiriwa na dawa za kulevya
☐ Kwa sasa situmii dawa za kulevya au dawa ambazo zinaweza kuathiri utendaji wangu

**KUMBUKA KWAMBA**

Kushindwa kuweka alama ya (√) kwenye visanduku vyote, itamlazimu dereva kutoendesha gari na atahitajika kuwasiliana na msimamizi au meneja wake mara moja.

Saini ya dereva

☐

**JEDWALI LA PILI**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 9(1))*

KIOLEZO CHA MPANGO WA USIMAMIZI WA MADHARA YA UCHOVU

Yaliyomo katika Mpango wa Usimamizi wa Madhara ya Uchovu

## 1. Utangulizi

- Jina la mtoa huduma
- Aina ya huduma zinazotolewa
- Lengo la Mpango wa Usimamizi wa Madhara ya Uchovu
- Mawanda (dereva na aina ya chombo kilichokusudiwa)

## 2. Utambuzi na Tathmini ya Madhara ya Uchovu

- Mbinu za kutambua madhara ya uchovu (kuripoti binafsi, uchunguzi, teknolojia)
- Sababu za madhara (muda mrefu wa kuendesha, zamu za usiku, kuto kulala usingizi na masuala ya afya)
- Zana za tathmini (tafiti, bangokitita la tathmini ya madhara ya uchovu)

## 3. Mikakati ya Kudhibiti Uchovu

- Kupanga utaratibu:
    - Ukomo wa masaa ya kuendesha chombo.
    - Mapumziko ya lazima na vipindi vifupi vya mapumziko
    - Sera ya mzunguko wa kazi.
- Usimamizi wa wingi wa kazi
- Kuhamasisha utaratibu wa kulala usingizi wa kutosha
- Udhibiti wa mazingira (mf, kuwepo hewa na mwanga wa kutosha nadi ya chombo)
- Matumizi ya teknolojia ya kugundua uchovu (mf, mifumo ya ufuatiliaji wa uchovu, vifaa vya kugundua hatari)

## 4. Mafunzo ya ufahamu wa uchovu kila robo mwaka kwa madereva na wasimamizi

- Elimu kuhusu dalili na viashiria vya uchovu
- Mwongozo juu ya uchaguzi wa maisha yenye afya kupambana na uchovu
- Mafunzo ya matumizi ya vifaa vya kutambua uchovu

## 5. Ufuatiliaji wa Madhara ya Uchovu na Utoaji wa Taarifa

- Utaratibu kwa madereva kuripoti uchovu
- Mifumo ya ufuatiliaji (kamera, vitambuzi vya ndani ya chombo).

- Kuripoti matukio yanayohusiana na uchovu
- Mapitio ya mara kwa mara ya matukio yanayohusiana na uchovu na makosa hatarishi

**6. Udhibiti wa Matukio ya Uchovu**

- Utaratibu wa kusimamia madereva waliochoka wakiwa kazini
- Hatua za haraka (mf, mapumziko kwa madereva, kubadilishana uendeshaji)
- Uchunguzi wa matukio na uchambuzi wa chanzo
- Hatua za urekebishaji na ufuatiliaji

**7. Utunzaji wa Kumbukumbu na Nyaraka**

- Kazi za dereva na kumbukumbu za kupumzika
- Tathmini ya madhara ya uchovu
- Kumbukumbu ya mafunzo
- Ripoti za matukio yanayohusiana na uchovu
- Kupitia na kukagua taarifa za ufanisi wa Mpango wa Udhibiti wa Madhara ya Uchovu (FRMP)

**8. Mapitio na Uboreshaji Endelevu**

- Ratiba ya mapitio ya mara kwa mara ya FRMP
- Maoni kutoka kwa madereva na usimamizi
- Kuhuwisha sera na taratibu kulingana na matokeo
- Kuunganishwa na mifumo ya jumla ya usimamizi wa usalama

**9. Uwezeshaji na Rasilimali**

- Upatikanaji wa huduma za tathmini na matibabu kwa madereva
- Programu za usaidizi kwa wafanyakazi (EAP) kwa masuala ya afya yanayohusiana na uchovu
- Mawasiliano na waratibu wa usimamizi wa madhara ya uchovu au wataalamu wa afya

**JEDWALI LA TATU**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 18(2))*

KIWANGO CHA ADHABU ZILIZOFIFISHWA

| **Na.** | **Makosa** | **Kanuni** | **Onyo** | **Adhabu iliyofifishwa** |
|---|---|---|---|---|
| | MAKOSA KWA MTOA HUDUMA | | | |
| 1 | Kushindwa kutekeleza na/au ukiukaji unaorudiwa wa Mpango wa Kudhibiti Madhara ya Uchovu ulioidhinishwa | 10(e) | | 100,000/= |
| 2 | Kushindwa kumpumzisha dereva, ambaye masaa yake ya kuendesha chombo yamepita | 10(g) & (h) | | 100,000/= |
| 3 | Kuruhusu dereva mwenza kuwa ndani ya chombo cha masafa marefu wanachotarajia kubadilishana | 10(k) | | 100,000/= |
| 4 | Kamera ya kugundua uchovu haifanyi kazi vizuri wakati wote chombo kinapokuwa safarini | 10(l) | | 100,000/= |
| | | | | |
| | MAKOSA KWA DEREVA | | | |
| 5 | Kuripoti kazini na kuendelee na safari wakati dereva anafahamu kuwa ni mchovu | 12(a) | | 50,000/= |
| 6 | Kushindwa kutunza na kutumia ipasavyo Kitufe cha Utambuzi (I-burton) wa dereva | 12(b) | | 50,000/= |
| 7 | Kushindwa kukabidhi chombo kwa dereva mwenza katika sehemu iliyoainishwa kwenye Mpango wa Kudhibiti Madhara ya Uchovu | 12(e) | | 100,000/= |
| 8 | Kuto kuzingatia muda wa kupumzika kama ilivyoainishwa chini ya kanuni ya 8 ya Kanuni hizi | 12(f) | | 50,000/= |

## JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 19)*

ELIMU KUHUSIANA NA MADHARA YA UCHOVU

| Na. | VISABABISHI | ZUIO |
|---|---|---|
| 1 | Kuto kulala usingizi wa kutosha na usio wa kawaida | Zingatia nidhamu ya kulala usingizi (masaa 6 hadi 8) |
| 2 | Matumizi ya pombe na dawa nyingine za kutuliza | Fanya vipimo vya kilevi na dawa za kutuliza kabla ya kuendesha chombo |
| 3 | Msongo wa mawazo na wasiwasi | Kuhimiza upimaji wa mwili na ufahamu juu ya afya ya akili |
| 4 | Magonjwa sugu | Fanya uchunguzi wa afya na matibabu mara kwa mara |
| 5 | Utaratibu mbaya wa kula na upungufu wa maji mwilini | Hakikisha dereva anakula chakula kinachofaa na kunywa maji ya kutosha |
| 6 | Sababu za mazingira | Hakikisha mazingira mazuri ya kazi |
| 7 | Muda mrefu wa kufanya kazi | Zingatia mahitaji ya saa za kazi na muda wa kupumzika |

Dodoma

……………………., 2025

…………………………….
*Makame M. Mbalawa*
*Waziri wa Uchukuzi*